

**MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI (CMT) KILICHO FANYIKA
TAREHE 19/04/2022 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA
MAGU KUPITIA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KUTOKA IDARANI**

“KIZIDUO”

WAJUMBE WALIOHUDHURIA;

1	Bw. Wilbard Bandolla	Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)	Mwenyekiti
2	Bw. Henry Sadatale	Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala	Katibu
3	Bi. Godfreda Masale	Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika	Mjumbe
4	Bw. Francisco M. Ndazi	Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki	Mjumbe
5	Bi. Grolly V. Mtui	Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi	Mjumbe
6	Bw. James Malima	Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari	Mjumbe
7	Bi. Lelesia J. Nyakahinga	Kaimu Mkaguzi Mkuu na Mthibiti Ubora wa Shule	Mjumbe
8	Bi. Emmanuela Chacha	Kaimu Katibu TSC	Mjumbe
9	Bw. Maigu Gisema	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi	Mjumbe
10	Bw. Medardy Majula	Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi (W)	Mjumbe
11	Bw. Mohamed Kyande	Mkuu wa Idara ya mifugo na Uvuvi	Mjumbe
12	Bw. Kishosha Masele	Afisa Mapato	Mjumbe
13	Bw. Mwagala Masunga	Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi	Mjumbe
14	Bw. Phabia Kabambala	Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Ufuatiliaji na Takwimu	Mjumbe
15	Eusebius Chanjali	Kaimu Mganga Mkuu (W)	Mjumbe
16	Adv. Merchades Rusasa	Kaimu Mkuu wa Kitengo Sheria	Mjumbe
17	Bw. Julius Ndyanabo	Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara	Mjumbe
18	Bi. Shida K. Misana	Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana	Mjumbe
19	Bw. John Bosco B. Joseph	Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira na Uthibiti wa Taka Ngumu	Mjumbe
20	Bw. Wilfred Majigo	Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili	Mjumbe
21	Bw. Festus Kisanga	Kaimu Afisa Biashara	Mjumbe

SEKRETARIETI:

- | | | |
|---|---------------------|--------------------|
| 1 | Bw. Simion Mwita | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Bw. Martine E. Maya | Mwandishi wa Vikao |

MUHT. NA. 107/2021/2022: - KUFUNGUA KIKAO.

Katibu wa Kikao alimkaribisha mwenyekiti ili afungue kikao baada ya kujiridhisha na akidi ya wajumbe kwenye kitabu cha mahudhurio.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao cha kawaida kwa ajili ya kupitia Taarifa za utekelezaji miradi ya maendeleo kipinid cha Januari – Machi, 2022 pamoja na taarifa ya mapato na matumizi kuishia tarehe 31/03/2022. Alifungua kikao saa 2.34 asubuhi.

MUHT: NA.108/2021/2022: - KURIDHIA AGENDA

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuzipitia agenda zilizoandaliwa kwa ajili ya kikao kama ifuatavyo:

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichofanyika tarehe 14/03/2022.
4. Yatokanayo na kikao kilichofanyika tarehe 14/03/2022
5. Taarifa ya mapato na matumizi kuishia tarehe 31/03/2022
6. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kipindi cha Januari – Machi, 2022
 - Elimu, Afya na Maji
 - Uchumi, Ujenzi na Mazingira
 - Fedha, Uongozi na Mipango
 - UKIMWI (CMAC)
7. Maombi ya kuhamisha mizinga ya nyuki kumi na tano (15) toka Bomani
8. Taarifa ya wafanyakazi Hodari 2022
9. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya UVIKO-19 ujenzi wa nyumba ya watumishi Hospitali ya Wilaya ya Magu
10. Mengineyo
11. Kufunga kikao

MUHT. NA 116/2021/2022:- TAARIFA YA UTEKELEZAJI MIRADI YA UVIKO-19 UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI HOSPITALI YA WILAYA YA MAGU YENYE THAMANI YA TSHS 90,000,000/=


Mkuu wa Idara ya Afya aliwasilisha taarifa ya ujenzi wa nyumba ya watumishi ya (three in one) tatu kwa moja yenye thamani ya Tshs 90,000,000/=, nyumba iko kwenye hatua ya ukamilishaji wa mwisho (*Taarifa imeambatanishwa*).

Wajumbe waliipokea taarifa na kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha hizo ambazo zitasaidia upungufu wa nyumba za watumishi Hospitali ya Wilaya ya Magu.

MUHT. NA 118/2021/2022: - KUFUNGA KIKAO

Katibu wa kikao alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao katika kikao, alishauri maazimio yaliyofikiwa yote yafanyiwe kazi, alifunga kikao hicho saa 9.30 Alasiri.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA


.....
KATIBU


.....
MWENYEKITI

TAREHE ~~28~~ 05/03/2012
.....

MKOA MWANZA

01: MAGU

MKOA	HALMASHAURI	JINA LA MRADI	JINA LA KITUO/SHULE	IDADI YA MIUNDOMI BINU	KIASI KILICHODHINISHWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOPOKELEWA	KIASI KILICHOTUMIKA	MAGU KWA FEDHA ZA MKOPO WA IMF				ASILIMIA YA UTEKEL EZAJI		
								HATUA YA ASILIMIA	KUTA	MISINGI	KUEZEKA			
MWANZA	MAGU	Ujenzi wa Nyumba ya watumishi katika Hospitali ya Wilaya	MAGU	1	90,000,000.00	90,000,000.00	85,539,632.00	MATUMIZI	HAUJA ANZA	0	0	1	96	
							JUMLA							
							1	90,000,000.00	90,000,000.00					